inayoendana na maumbile, tabia zao za asili na hali bora.

Mfumo wa uzalishaji, usambazaji na biashara wenye uwazi, haki na uwajibikaji kwa mazingira na jamii unahitajika ili kujenga usawa na haki.

### 2.4 Kanuni ya uangalizi

Kanuni hii inasema kwamba tahadhari na uwajibikaji ni masuala muhimu sana katika kusimamia, kuendeleza na kuchagua teknolojia za kilimohai. Sayansi ni muhimu katika kuhakikisha kwamba kilimohai ni mfumo sahihi kiafya, kiusalama na kimazingira. Hata hivyo, maarifa ya kisayansi pekee hayatoshi. Bali uzoefu wa kiutendaji, hekima, busara na ubunifu uliojengeka kwa miongo kadhaa husaidia katika kutatua matatizo ya aina mbalimbali ya kiuzalishaji na muendelezo. Kilimohai lazima kizuie athari za wazi zinazoweza kujitokeza kwa kubuni na kutumia teknolojia sahihi. Pia kukataa teknolojia zisizokuwa endelevu ambazo athari zake hazijafahamika bayana kama vile ya viini tete (GMO).



TOAM
Tanzania Organic Agriculture Movement

Maamuzi lazima yazingatie amali na mahitaji ya wote wanaoweza kuathirika, kwa kutumia mchakato ulio wazi wa ushirikishwaji jamii. Kilimo hai kinatoa tahadhari na uwajibikaji unaoweka kinga kwa afya na ustawi wa vizazi vya sasa na vijavyo pamoja na kujali mazingira endelevu

**Angalizo:**

*Hii ni tafsiri ya kanuni za kilimohai kama zilivyoainishwa na kuidhinishwa na IFOAM katika lugha ya kiingereza. Makosa yote ya tafsiri ni jukumu la mtafsiri na si la IFOAM au TOAM kama taasisi.*

**Imetafsiriwa na: Bakari Mongo**
Mtendaji Mkuu-TOAM
P.O. Box 70089 Dar es Salaam, Tanzania.
**Tel:** +255 (0) 744134999 or +255 (0) 710267652
**Email:** toam@kilimohai.org
**Website:** www.kilimohai.org



TOAM
Tanzania Organic Agriculture Movement

### 1.0 Maana ya Kilimohai

Kilimo hai (organic farming) ni aina ya kilimo kinachohusisha shughuli zote zinazofanyika katika uzalishaji wa bidhaa na mazao ili kukidhi mahitaji yetu kwa kuzingatia kanuni za msingi na viwango vilivyoainishwa.

**1.1 IFOAM** inatafsiri kilimohai kuwa ni mfumo wa uzalishaji unaojali/zingatia na kuendeleza rutuba katika udongo, ikolojia pamoja na ustawi wa watu. Unategemea mchakato wa kiikolojia, bayoanuai na hali ya kimazingira kuliko kutegemea matumizi ya pembejeo zenye kuleta madhara. Kilimohai kinahusisha ujuzi na maarifa ya asili, ubunifu na utafiti wa kisayansi katika kuinua uzalishaji wa kuhimiza utunzaji mazingira, kuhuisha usawa na haki na kuboresha hali ya Maisha.



**1.2** **FAO** inatafsiri kilimohai kuwa ni sehemu ya kilimo endelevu kinachohusisha mbinu Rafiki zenye kuhifadhi mazingira na zinazowezesha uzalishaji wa mazao na mifugo pasipo kusababisha madhara au uharibifu katioka ikolojia ya shamba, rutuba ya udongo, uwepo wa maji, bayoanuai na maliasili zinazozunguka shamba. Dhana ya kilimohai inazingatia kizazi cha sasa na vijavyo kwa kuhifadhi na kuboresha mali asili badala ya kuziharibu na kuzimaliza.

**1.3** **Codex Alimentarius Commission** pia imemtafsiri kilimohai kuwa miongoni mwa njia nyingi zinazosaidia hifadhi ya mazingira. Mfumo wa kilimohai umeweka kanuni na viwango mahususi vinavyopaswa kuzingatiwa wakati wa uzalishaji kwa lengo la kuhuisha ikolojia na uendelevu wa mazingira na jamii.

Neno kilimohai au organic linatumika kutambulisha bidhaa iliyozalishwa kwa kuzingatia viwango na kanuni za kilimohai na kupata uthibitisho wa hati na alama kutoka kwa mamlaka ya udhibiti ubora na viwango.

## Utangulizi wa kanuni za kilimohai

Kanuni hizi ndio msingi wa kilimohai na mchango unaoweza kuifanya dunia kuboresha kilimo kwa ujumla. Kilimo ni moja ya shughuli muhimu zinazofanywa na binadamu kwa ajili ya kupata mahitaji ya kila siku ili kujikimu.

Kanuni zinazotumika katika kilimo kwa ujumla zinahusisha mtazamo wa watu juu ya udongo, maji, mimea na Wanyama katika kuzalisha, kuandaa na kusambaza chakula na bidhaa nyinginezo. Zinaonesha namna watu wanavyoona uhai na mandhari ya ardhi, mahusiano miongoni mwao na mwelekeo wa matumaini kuhusu vizazi vijavyo. Kanuni za kilimohai zinatoa mwongozo katika kuweka viapumbele juu ya maendeleo, mipango na viwango na kuwakilisha mtazamo wake kidunia.

## 2.0 Kanuni za msingi za kilimohai.

Kuna kanuni kuu nne za msingi wa kilimohai kama zilivyofafanuliwa na IFOAM;

1. Kanuni ya Afya
2. Kanuni ya Mazingira
3. Kanuni ya Haki na Usawa
4. Kanuni ya Uangalizi

### 2.1 Kanuni ya Afya

Kanuni hii inaonyesha kwamba afya ya watu au jamii haiwezi kamwe kutenganishwa na afya ya kimazingira. Ardhi yenye afya huzalisha mazao bora kwa afya na uhai wa binadamu na wanyama. Kilimohai sharti kiwe endelevu kwa kuzingatia urutubishaji udongo na kuboresha afya ya mimea, wanyama na binadamu katika dunia bila utengano wa aina yoyote. Afya ni mfumo wa uhai na utaratibu wa maisha kwa ujumla unaozingatia siyo tu kutokuwepo kwa magonjwa bali kuujali na kuutunza mwili, akili, ustawi wa jamii na mazingira bora na mazuri ya kuishi. Uwezo wa kujikinga kushiriki katika uumbaji na kujijali ni tabia ya msingi na muhimu kwa afya bora.

Kilimohai kinalenga kuzalisha chakula bora ambacho huchangia kuboresha kinga na ustawi wa afya ya mlaji. Kwa mtizamo huu, shughuli za kilimohai zinaepukana na matumizi ya mbolea za kemikali, viuatilifu, madawa ya mifugo na virutubisho ambavyo vinaweza kuwa na madhara kwa mtumiaji.

Kwa hakika kilimohai kinalenga katika uzalishaji wa chakula kinachokidhi viwango vya ubora na usalama wa hali ya juu ili kuchangia katika kujikinga na kujenga siha nzuri. Kwa kuzingatia afya, usalama na uhai, kanuni za kilimohai zinazuia matumizi ya mbolea, madawa ya wadudu au magonjwa ya mifugo na viatilifu au vinasaba vinavyoongezwa katika hifadhi ya vyakula ambavyo vinaweza kusababisha madhara ya kiafya kwa mlaji au mtumiaji.

### 2.2 Kanuni ya mazingira

Kanuni hii inawezesha kilimo hai kuhuisha na kuhifadhi mazingira. Inaweka mkazo katika uzalishaji unaolenga na kutegemea mfumo endelevu wa kimazingira. Hali bora na ustawi hupatikana kutokana na mazingira ya uzalishaji yanayojali uhai wa viumbe wengine. Kwa mfano, uzalishaji wa mazao unapaswa kuzingatia na kujali urutubishaji wa udongo, ufugaji wanyama unaozingatia mfumo wa kimazingira wa shamba, ufugaji wa samaki na viumbe hai wa baharini uzingatie mfumo wa mazingira ya bahari.

Pamoja na kuwa kilimohai kinaendana na mazingira ya kawaida na tamaduni za mahali popote duniani kwa kuzingatia kanuni za msingi, matumizi ya pembejeo sanisi/kemikali sharti yapungue na kuongeza ufanisi wa matumizi ya rasilimali na maliasili pale inapowezekana kurejeshwa upya na kutumika tena.

Kilimohai lazima kifanikishe uwiano wa kimazingira kwa kubuni na kuhimiza mfumo wa uzalishaji unaoweka mazingira bora kwa makazi na kutunza anuai za vina saba na kilimo. kwa wadau wote wa mnyororo wa thamani.

### 2.3 Kanuni ya haki na usawa

Kanuni hii inasisitiza kwamba, wale wote wanaojihusisha na kilimo hai ni lazima wazingatie mahusiano yenye usawa katika ngazi zote bila upendeleo, iwe ni wazalishaji, walaji, wasindikaji, wafanyakazi, wafanyabiashara au wasambazaji ili kuhuisha na kuboresha mazingira na kuhifadhi maliasili na rasilimali. Kilimo hai lazima kilete uwiano na urari wa kimazingira kwa kubuni na kuhimiza mfumo wa uzalishaji unaoweka mazingira bora kwa makazi na kutunza rasilimali katika jitihada za kuendeleza kilimo. Wazalishaji, wasindikaji, wauzaji au wanunuzi, walaji na watumiaji wote wa bidhaa za kilimo hai wanapaswa kushiriki kikamilifu katika kukinga na kuzuia uharibifu wa mfumo mzima wa mazingira unaojumuisha mandhari, viumbe, bionuai, hewa na maji.

Kilimohai kinapaswa kuwapatia Maisha bora wale wote wanaojihusisha nacho na kuchangia katika uhakika wa chakula na kupunguza umaskini. Malengo ya kilimohai ni kuzalisha chakula na bidhaa za kutosha kwa kuzingatia viwango vya ubora. Kanuni inasisitiza kuwa wanyama lazima wapatiwe fursa na hali ya kimazingira